

Public education
Discover a world of opportunities

NAMBA: KUSOMEA NYUMBANI

KUTAMBUA HESABU


Hapa ni baadhi ya mawazo ya kukusaidia kuweza kuleta hesabu katika maisha ya mtoto wako:

- Fikiria kwa upana wakati unatumia hesabu, wakati, nafasi na vipimo ili mtoto wako aone jinsi ambavyo hesabu inaweza kuwa ya mhimur. Kwa mfano: *Nashangaa kama tuna mapera ya kutosha? na ngoja tuhesabu ili kuhakikisha.*
- Mtie moyo mtoto wako ndivyo aweze kuzungumza kile mnachokifanya. Uliza maswali na ruhusu mtoto wako kuuliza maswali pia. Hii inasaidia kuelewa vitu na kuwasaidia vile wanavyovifanya. Ni njia nzuri yakujifunza.
- Kulinganisha na kuamuru urefu wa vitu ndani na kuzunguka kwa nyumba. Kwa mfano: *Ni chombo kigani kirefu zaidi? Ni soksi gani ndefu zaidi? na unaweza kupanga vikombe hivi kwenye mpangilio kutoka vifupi mpaka virefu?*
- Watie watoto wako moyo kusoma gazeti, kwa mfano wanaweza kutafuta vitu vyote vya gharama chini ya \$5(tano) Uliza maswali kama: *Ni makopo mangapi tunaweza kununua na \$10 (kumi)? na Kama ungekuwa na \$50 (hamsini) ya kutumia, ni nini unaweza kununua kwa hiyo pesa?*
- Watie moyo kugundua na kutumia mwelekeo katika mazingira, kwa mfano mtindo kwenye makaratasu ya kufungia vitu, samani, shanga na mavazi. Kuunda ruwaza kutoka shanga na vitalu.

Zima televisheni. Ni rahisi mtoto kuweza kutulia kama hakuna vitu vingine vya kumhangisha.

- Uliza maswali wakati wewe unafanya shughuli za kila siku ili waweze kuanza kufikiria na kuzungumza kuhusu hesabu kuanzia umri mdogo. Uliza maswali kama vile: Ni wangapi huko? Hii ni njia ipi? Je itaenea pale? Je, kuna za kutosha sisi wote? na Ni kubwa kiasi gani?
- Msifie mtoto wako kwa kujaribu, hata kama jibu si la ukweli. Kama hawajui majibu, wape mda wa kutafakari. Kama ukiwambia jibu, waelezee jinsi ulivyolipata. Hii inajenga kujiamini katika kusoma. Wape mda wa kufikiri na mda wa kujibu maswali yako. Uwe mvumilivu.

Fuata sheria ya dhahabu ya ‘kidogo na mara kwa mara – dakika chache kila siku akijifunza hesabu ni bora kuliko dakika 30 za hisabati.



Department of
Education

**Utapata zaidi
Kijitabu cha ukweli cha kusomea nyumbani
Kwenye elimu hapo: education.wa.edu.au.**